



## TAARIFA KWA UMMA

### UGAWAJI WA MASHINE ZA EFD BILA MALIPO AWAMU YA KWANZA KWA WAFANYABIASHARA WA KATI NA WADOGO MKOA WA DAR ES SALAAM:

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwataarifu Wafanyabiashara wote kwamba, zoezi la ugawaji wa Mashine za EFD awamu ya kwanza kwa Wafanyabiashara wa Kati na Wadogo litafanyika kwa utaratibu ufuatao.

- Katika awamu ya kwanza tutaanza kugawa Mashine za EFD kwa Wafanyabiashara wachache wa Mkoa wa Dar es salaam wapatao **5,703**.
- Wafanyabiashara hao **5,703** ni wenye mauzo ghafi kati ya Shilingi **milioni 14** na **milioni ishirini (20)** kwa mwaka.
- Wafanyabiashara wa kundi hilo wafike katika ofisi za Mamlaka ya Mapato za Mikoa wanayolipia kodi ya Ilala, Kinondoni na Temeke ili kuhakiki usajili wao wa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN), na kupata kibali cha kupewa Mashine ya EFD kuanzia **tarehe 01 Juni 2016**.
- Wafanyabiashara watatakiwa kwenda na nakala ya cheti cha TIN, Picha mbili ndogo (Passport size), Leseni ya biashara, namba ya simu ya kiganjani, na maelezo kamili ya sehemu wanayofanyia biashara, kama jina la mtaa, namba nyumba na au jina la eneo maarufu liliopo karibu na wanapofanyia biashara.

- Baada ya kupata kibali Mfanyabiashara atakwenda kuchukua Mashine ya EFD kutoka kwa mmojawapo wa Wasambazaji wa EFD walioidhinishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ambao ni wafuatao:-  
  
(1) Pergamon Group Ltd, (2) Bolsto Solutions Ltd, (3) Advatech Office Supplies Ltd, (4) Compulynx Tanzania Limited, (5) Web Technologies Ltd, (6) Softnet Technologies Limited, (7) Maxcom Africa Limited na (8) Power Computers and Telecommunication Limited.
- Mfanyabiashara ataingia mkataba wa huduma baada ya mauzo na Msambazaji kwa ajili ya kupewa huduma ya matunzo na matengenezo ya Mashine ya EFD.

Wafanyabiashara wa Mkoa wa Dar es salaam watakaobaki na wale wa Mikoa mingine Nchini wanaostahili kupewa Mashine za EFD bila malipo watapewa Mashine hizo katika awamu ya pili.

Tunapenda kuisitiza kwamba, Wafanyabiashara wote wanaotakiwa kutumia Mashine za EFD kutunza kumbukumbu za biashara na kutoa risiti, watumie Mashine hizo kikamilifu na ipasavyo kwa hiari bila kushurutishwa.

Kwa maelezo zaidi piga kituo cha huduma kwa wateja namba **0800-780078**, **0800-750075** au kwa barua pepe **huduma@tra.go.tz**

*“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”*

**IMETOLEWA NA**

Alphayo J. Kidata  
**KAMISHNA MKUU**